**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OWM - TAMISEMI**
**HALMASHAURI YA MJI RUFIJI**
**SHULE YA SEKONDARI KAZAMOYO**

MAKAMU: +255756472805
MATRON: +255718 891828
MHASIBU: +255625300341
MWALIMU WA TAALUMA : +255625338063
Barua pepe: kazamoyosecschool2010@gmail.com /
kazeeramadhanigwimo@gmailcom

S.L.P 61,
IKWIRIRI-RUFIJI
PWANI

KUMB,NA. KZM SS/RFJ,VOL1/2026/03
MZAZI WA………………………………….
S. L. P ………………………………….

Yah: **<u>MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI KAZAMOYO HALMASHALIRI YA MJI RUFIJI, MKOA PWANI MWAKA…………………..</u>**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka……………..na atasoma tahasusi ya………………

Shule ya Sekondari KAZAMOYO ipo umbali wa Kilometa 160 Kusini Arnwa Mji wa Dar es Salaam, Usafiri wa basi kutoka mjini Dar es Salaam unapatikana katika kituo cha mabasi **MBAGALA RANGI 3** Nauli ni Shilingi 8,000/= hadi **lkwiriri-Rufiji.**

Muhula wa Masomo unaanza tarehe……………hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shule ni tarehe………………Mwisho wa kuripoti ni tarehe…………….

## 2.0 Mambo muhimu ya kuzingatia: -

## 2.1 SAREZA SHULE

A. Sketi rangi ya **AQUATIC BLUE (BLUU BAHARI) 02** ndefu na ivuke magoti inch 5 au zaidi kwa kwenda chini, mshono linda box.
B. Sketi moja ya **BROWN ESTIM Namba moja** kwa ajili ya kushindia (shamba dress) na zitavaliwe baada ya vipindi vya darasani.
C. T-shirt moja yenye nembo ya shule utanunua Jirani na shuleni kwa gharama nafuu .

D. Nembo (logo) ya shule kwa ajili ya kuweka kwenye mashati /nusu kanzu za shule za shule.
E. Sare za michezo (Jezi) **(TRACK SUIT RANGI YA KIJIVU).**
F. Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba vya kufunika visiwe na visigino virefu (**Jozi 2)**
G. Shati nyeupe rnbili mikono mirefu ,nusu kanzu mbili na hijabu yake kwa wanaotakakuvaa hijabu
H. Soksi nyeupe jozi 2 au zaidi.
I. Viatu vya rnichezo (raba rangi yeyote) zisizo na urembo.
J. Kandambili (siyo yebo yebo) kwa ajili ya kuogea tu.
K. Hijabu rangi nyeupe au **BROWN KITAMBAA CHA HALUA** kwa ajili ya kushindia na sweta la **LIGHT BLUE.**
L. Tisheti (T-shirt) 2 rangi dark blue, **INAPATIKANA KWENYE MAZINGIRA JIRANI NA SHULENI IKIWA NA NEMBO YA SHULE**.

**N.B: Mwanafunzi awe amevaa sare ya shule wakati wa kuripoti .**

2: 2 . **MAHITAJI MENGINE**

A. Madaftari (**COUNTER BOOK)** Kuanzia **QUIRE 3,(Q3)** kwa masomo yake
B. Ream (A4) ya Karatasi bunda Mbili (2) kwa mwaka;
C. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (orodha imeambatanishwa);
D. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosorna Biology,
E. Scientific Calculator;
F. Aje na godoro la INCH ( 2.5 x 6). Lenye foronya au anaweza kutumia godoro la shule kwa kuchangia 20,000/= kwa mwaka.
G. Mashuka Jozi 2 (PINK ALI LIGHT blue), chandarua 1.
H. Nguo za ndani za kutosha;
I. Vyombo chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
J. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
K. Kwanja 1, dekio (mop) 1, rubber squeezer 1, reki -l, mifagio 2 wa ndani na nje .

## 2.3 MICHANGO MBALIMBALI:

a) Shule ya Bweni

| Na | Aina ya Mchango. | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 2. | Tahadhari | 5,000/= |
| 3. | Nembo | 5,000/= |
| 4. | Kitambulisho cha Shole | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/ =** |

**NB**: **Kwa muhula wa kwanza malipo yote yapitie benki yalipwe kwenye akaunti yenye namba ifuatayo**

**NAMBA 21301100063 NMB JINA LA AKAUNTI: KAZAMOYO SEKONDARY SCHOOL-RECURRENT.** Tsh 80,000/= kwa muhula wa kwanza au kwa awamu. Utapata huduma katika tawi lolote la Benki ya **NMB** Tanzania. Kumbuka kuwa makini katika kuweka fedha kwenye akaunti ya benki uliyopewa Shule haitahusika na uzembe wowote wa kuchanganya malipo katika akaunti ya shule, **Jina Ia mwekaji liwe la mwanafunzi** na ***si mzazi/mlezi***. Mwanafunzi aje na **PAY SLIP** ya benki yenye jina lake wakati wa kuripoti shuleni. Mwanafunzi anatakiwa kukamilisha malipo ya Michango kabla ya kuripoti shuleni na kupewa kadi maalumu ya utambulisho hapa shuleni.

**3:0 Sheria na Kanuni muhimu za Shule**

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa jumla ni jambo la lazima.
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya Shule kulingana na ratiba ya Shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku ( night Preparation) ni lazima;
iv. Mwanafunzi anatakiwa kuwahi katika kila Shughuli za shule atakazopangiwa;
v. Kufahamu mipaka ya Shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya Shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingaüa ratiba ya shule wakati wote,'
ix. Kutunza mali za shule,
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na walezi wa bweni.

xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili **dini** wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

1. Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;

2. Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa, Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa, Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;

3. Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa mkuu wa Shule. (ikiwa kumetokea dharura yenye ulazima wa Kwenda nyumbani ) .

3.2. **Makosa yatakayosababisha mwanafunzi kufukuzwa shule ni pamoja na:**

i. Wizi;

ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro,"
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo shuleni.
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule,
vi. Kusuka nywele kwa mtindö usiokubalika, Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa USUSI uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu,Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya; Uvutaji wa sigara;
viii. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa.
ix. Kupata ujauzitö au kutoa mimba;
x. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xi. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni.
xii. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule
xiii. Kudharau Bendera ya Taifa;
xiv. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu
xv. Uharibifu wa mali ya urnrna kwa makusudi.

4. **Viambatisho na Fomu Muhimu**.

i. Fornu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali,
ii. Fornu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fornu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotole wa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu

**Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

**KARIBU SANA KATIKA SHULE YA SEKONDARI KAZAMOYO**

Saini ya Mkuu wa Shule

Jina la Mkuu wa Shule: **Ramadhani Haruna Kazee**

Mhuri wa Mkuu wa Shule .

NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa**. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO:**

Makamu Mkuu wa Shule 0756472805

- Mwandamizi Taaluma 0654489566/0683842209
- Mwandamizi Malezi 0787194760.
- Mwalimu wa bweni 0718891828.
- Matron. 0622739224.

**OWM - TAMISEMI**
**HALMASHAURI YA MJI RUFIJI**
**SHULE YA SEKONDARI KAZAMOYO**

MAKAMU MKUU WA SHULE+255756472805
MHAS1BU. +255625300341

S. L. P 61,
**Barua pepe**: kazeeramadhanigwimo@gmailcom
IKWIRIRI – RUFIUI
PWANI

## MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI

Jina la mwanafunzi…………………………….adm.Na………Kidato……..mchepuo…. mwaka....**.....**Tarehe ya kuzaliwa………….Mahali ulipozaliwa.............Kabila………….Uraia wa mwanafunzi..... Tarehe ya kuliunga na Shule ya sekondari ya **kazamoyo** Shule aliyotoka ya kidato I-IV **…………….**Masomo utakayokuja kusoma. ..................................... Kama ni mlemavu,taja aina ya ulemavu……………………….Je unarudia kidato?Toa sababu?.....................................................................................................................
...........................................................................................................................
.................

Dini ya mwanafunzi…………………Dhehebu ……………………….…………

Anuani ya kudumu ya mwanafunzi ……………… S.L.P …………. Wilaya ……………….

Mkoa………………Tarafa …………... Kijiji/mtaa …………… Namba ya nyumba …… Simu ya nyumbani …………………….. simu ya kazini/ofisini ……………………

BABA

Jina la Baba……………..…………..Je? yupo hai? …………

Kabila la baba ………………

Anwani yake ya sasa ……………………

kazi yake ………………………………..Mwajiri wake…………………………. Dini ya Baba ………………………..Dhehebu ………………… Je, Baba na Mama Wanaishi pamoja?............................ simu ya Baba …………………… ya kazini / ofsini ……………………..

**MAMA**

Jina la Mama………………………..Je? yupo hai? …………

kabila la Mama ………………

Anwani yake ya sasa ……………………kazi yake ………………………………..Mwajiri wake……………………………. Dini ya Mama ………………………..Dhehebu ………………… Je, Mama na Baba Wanaishi pamoja?............................. simu ya Mama …………………… sinu ya kazini/ ofsini ……………………..

**MLEZI**

Jina la Mlezi………………………. ………… kabila la mlezi …………………

Anwani yake ya sasa ……………………kazi yake ………………………………..Mwajiri wake……………………………. Dini ya Mlezi………………………..Dhehebu ……………

Uhusiano na mwanafunzi ?................................ simu ya mlezi………………… ya kazini/ ofsini ndugu wengine kama wapo ………….. ……………..

| SN | JINA | ANWANI | SIMU | UHUSIANO |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |

**PICHA ZA NDUGU WENGINE**

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | |

**TAARIFA NYINGINEZO KAMA ZIPO**

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

Sahihi ya mwanafunzi ………………………………… Tarehe ……………………………….

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

**PART "A"**

**FROM………………………………….**

**TO THE MEDICAL OFFICER**

**Mr/Mrs……………………………………………………………… Name in full**

Please examine the above named as to her physical and mental fitness for a full time student. The examination should include the following categories (l - Ill) each category or subcategory of which Will render the applicant ineligible in case of a defect Pregnancy (category IV) Will also render a girl student ineligible for studies.

I. (a) Eye sight (e) Venereal Diseases (b) Hearing (f) Leprosy

(c) Speech. (g) Epilepsy (d) Limbs

Il. Neuroses

Ill. Other serious diseases

**Date**……………………………… **Signature**……………………………

**PART B**:

**MEDICAL CERTI FICATE**

(To be completed by a Government Medical Officer)

I have examined the above named and consider that he/ she is physically fit/unflt and mentally fit unfit for a full time student.

I. (a).Eyesight.................................

(c) Venereal diseases ………………….

(b).Hearing………………………

(d)Limb………………………

(e)Leprosy ……………….

(f).Speech………………………………………………………………………

II. Neuroses…………………………………………………………………………

III. Other serious diseases……………………………………………………………...

IV. Pregnancy…………………………………………………………………

V. Date……………………signature……………station……………........

Designation…………………………………………………………………

E. **AHADI/ KIAPO CHA MWANAFUNZI**

Mimi ........................................................................................ Ambaye nimechaguliwa kujiun
ga na SHULE YA SEKONDARI KAZAMOYO KIDATO CHA TANO Mchepuo wa PCB mwaka 2026/2027 ninapokea na kuikubali nafasi niliyo pewa kwa malengo ya kusoma kwa bidii na kufikia malengo yaTaifa na Shule ya Sekondari ya bweni Kazamoyo.

Ninatambua kuwa nafasi hii ni adimu, nyeti na ya upendeleo kwangu ili niweze kusoma na kufanya vizuri katika masomo nikiwa na tabia na mwenendo mwema kwa ajili ya taifa langu la Tanzania, familia yangu na kwa ajiliyangu pia.
Nina amini kuwa vitendo vyovyote vinavyopelekea uzembe katika kufanikisha makusudio ni hujuma kwa Taifa langu, familia yangu na kwangu pia- HIVYO ninaahidi kuwa, nikiwa hapa shuleni: Nitasoma Kwa bidii kwa malengo ya kufanya vizuri katika masomo niliyo changuliwa kusoma

ii. Nitashika na kufuata sheria na taratibu zote za Shule kama nilivyo zisoma na kuzielewa na zingine zitakazo kuwa zikitolewa mara kwa mara

iii. Sitajihusisha na vitendo vyovyotevya utovu wa nidhamu nikiwa hapo shuleni.

iii. Nitasoma kwa bidii ili nifaulu masomo yangu yote kwa Daraja "A" **DIVISION ONE**

iv. Ikiwa nitakiuka sheria kanuni na taratibu za Shule kama nilivyo zisoma na kuzielewa, nitakubali kurudi nyumbani kumwita mzazi/ mlezi wangu (Jina la mzazi)………………………………….. Kwa ajili ya hatua zaidi. Saini ………..…Jina la mwanafunzi …………………………… tarehe ……………………

## SEHEMU YA MZAZI/MLEZI

Mimi ______________________ ninakubali mtoto wangu __________________________
Kupata na kupokea nafasi katika Shule ya sekondari KAZAMOYO mwaka 2026. Ninaahidi kumpatia mahitaji yote ya Shule kama ilivyo katika rnaagizo ya kujiunga na shule. Ninakuhakikishia kuwa nitashirikiana na shule wakati wote kuona kuwa mwanangu anatekeleza wajibu wake kwa Shule na kwa taifa. Anuani yangu ya kudumu ni ______________
Simu . __________________________ Iwapo nitapata uhamisho wa kubadili makazi nilazima nitaijulisha Shule kwa maandishi.

Jina la Mazazi/Mlezi ……………………… Saini …………. tarehe

**"TAFADHARI SOMA KWA MAKINI MAELEZO/MAAGIZO HAYA NA KUYATEKELEZA KIKAMILIFU"**

## VITABU

Kila Mzazi/Mlezi amnunulie mwanafunzi nakala moja wapo kwa kila somo na vilevile ahakikishe amemnunulia vitabu vifuatavyo:

## BIOLOGY

**i/** Biological Science by DJ Tylot

ii. Biology for advanced level secondary schools TIE ii.

iii.Understanding Biology for Advanced By Grenn&Sus an

iii. Advanced Biology Principles and Application by C.J. cleggand DG Mackean

## CHEMISTRY

i. Inorganic chemistry by TIE
ii. Physical chemistry Vol I &Il
iii. Physical Chemistry by Chand
iv. Organic chemistry TIE

## PHYSICS

i. Physics for advanced level secondary schools' students' book, form five, Tie
ii. Principle of physics,for A-level

## ACADEMIC COMMUNICATION

Academic communication for secondary school form five TIE

## HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI

Historia ya Tanzania na Maadili , Shule za Sekondari . (kitabu cha mwanafunzi) TaasiSi ya Elimu Tanzania.